

[Home](#) > [Sheria za Kiislamu Katika Dunia ya Kisasa](#) > [Mabadiliko katika Kilichotukia](#) > Binadamu na Mahitaji ya Zama

Mabadiliko katika Kilichotukia

Ustawi, ufanisi, maendeleo, mabadiliko na mageuzo ya historia ni katika mahitaji ya kimsingi ya maisha ya binadamu. Historia ya binadamu inabadilika lakini hakuna mabadiliko yoyote katika maisha ya mnyama yeyote au viumbe vya kijamii kama vile nyuki. Maisha na tabia ya nyuki haikubadilika. Kwa mfano, maandishi ya miaka elfu kadhaa iliyopita juu ya maisha ya nyuki yanathibitisha kwamba muundo na hali ya maisha ya nyuki ilivyo leo ni kama vile ilivyokuwa zamani.

Lakini kinyume chake, miundo na hali ya maisha ya binadamu kila siku inabadilika. Siri ya jambo hili linabainishwa na Qur'ani wakati inaposema kwamba binadamu ni kiumbe wa pekee ambaye yeye mwenyewe tu ndiye mwenye jukumu juu ya maisha yake. Hii ina maana kwamba viumbe vingine hata vile viumbe vyenye kuishi kijamii – maisha yao yanaongozwa na kusimamiwa na maumbile.

Silika ndiyo inayodhibiti maisha yao, wala viumbe havikupewa haki na uwezo wa kuingilia au kugeuza silika yao, wala havikupewa jukumu la kustawisha na kuendeleza maisha yao. Maisha yao yanafuata jinsi asili na maumbile yao yalivyokuwa tangu kuumbwa kwao. Lakini binadamu ni kiumbe anayeanzia katika udhaifu au sifuri na anaendelea katika mwendo wa kujikamilisha. Bila ya shaka mwendo wake hufuata miongozo ya Manabii na Mitume. Yeye mwenyewe ndiye mwenye jukumu la kujikamilisha binafsi. Ni lazima kwa binadamu kutumia akili, uwezo na jukumu lake ili ajikamilishe.

Kuhusu suala la mabadiliko ya maisha ya binadamu, kuna mambo kadha wa kadha ambayo kati yao baadhi yake mmeyasikia au mmeyasoma vitabuni. Tunapozungumzia suala hili, wapinzani wanasema: "Uislamu hautoshelezi zama zetu." Wabishi hao hutoa dalili moja ya kifalsafa ambayo inasema kwamba kanuni asilia ya ulimwengu huu hubadilika na iko katika mwendo (harakati). Hakuna hata kitu kimoja duniani ambacho kiko thabiti. Hakuna kitu kimoja katika nyakati mbili kiweze kuwa na hali moja na sawa. Sisi wenyewe ambao tumekaa hapa tukidhania kwamba kama tulivyokuwa jana ndivyo vivyo hivyo tulivyo hivi leo, kwa hakika leo yetu ikilinganishwa na jana yetu imebadilika sana, isipokuwa tu mabadiliko hayo hatuyahisi.

Tunapotazama akrabu inayoonyesha saa tunaona kuwa imesimama, na kila tukitazama zaidi hatuoni mwendo wowote, lakini baada ya saa moja tukitazama tena tutaona kwamba imekwenda 1/12 ya duara la uso wa saa. Kwa hivyo, kutoona kwetu mwendo wa saa hakumaanishi kwamba hakuna mwendo.

Maelezo mengi yametolewa kuhusu suala hili la asili na namna mwendo (harakati), mabadiliko na mageuko katika ulimwengu yalivyo. Wanafalsafa wa Kiislamu wanaamini kwamba johari (atomi) ina harakati, na kwamba maumbile ni sawa na harakati, hivyo yanabadilika.

Ikiwa kitu cha asili kabisa duniani, yaani maumbile, yanabadilika, hivyo hakuna kitu chochote chenye kuishi milele. Naam, dini ni mojawapo wa vitu au matukio ya dunia, hivyo dini haiwezi kubaki daima. Vitu vyote duniani haviwezi kuwepo tangu na tangu. Ikiwa tutaliangalia suala hili kwa mujibu wa nadharia ya kifalsafa tu, basi jibu lake litakuwa rahisi sana, nalo ni kwamba: Kile kinachobadilika na kugeuka ulimwenguni ni matukio ya dunia, yaani matukio au vitu vya kimaada au vya kidunia. Na hapana shaka yoyote kwamba matukio ya ulimwenguni yanageuka na kubadilika. Kwa mfano, Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w.w) mwenyewe ambaye ni tukio moja katika matukio ya ulimwenguni, alibadilika katika sura mbalimbali – alizaliwa mtoto mchanga, alikua tangu udogoni na akawa kijana, kisha mzee na hatimaye akafariki dunia. Qur'ani inasema:

"Kwa hakika wewe utakufa na wao (pia) watakufa." (Qur'an 39:30)

Mjadala wetu unahusu kanuni za dunia. Je, zinabadilika? Jua na mwezi vinakuwa vikongwe na siku moja vita angamia. Nyota, mimea, wanyama na viumbe vyote vya duniani vinakuwa vikuukuu na mwishowe vitaangamia. Lakini je, huu ni ushahidi wa kwamba kanuni za kifizikia au kimazingira nazo pia zinakuwa kuukuu? Uislamu wenyewe ni kanuni wala si tukio. Kila kinachobadilika ni tukio, walakini Qur'ani (yenye sheria za Kiislamu) ndiyo itakayobaki na Mtume atakufa. Mshairi mmoja amesema:

Mustafa aliahidi

Baada ya kutuahidi

Kwa Molaye atarudi

Kama wote maujudi

Ila tabaki abadi

Qur'ani Yake Mawdudi

Kwa viumbe kustafidi

Sheria ziso na hadi

Kuhusu Mtume Mtukufu, Mwenyezi Mungu anasema: ***"Kwa hakika wewe utakufa na wao (pia) watakufa."*** (39:30) Na kuhusu dini ya Kiislamu, anasema:

"Hakika Sisi tumeteremsha Kumbusho (Qur'ani), na hakika Sisi ndio tutakayoihifadhi." (Qur'an 15:9)

Qur'ani tunayoikusudia si haya makaratasi ya Msahafu ambayo yanachanika, yanafujika na yanaoza, bali ni ukweli na hakika ya Qur'ani.

Sheria za Kiislamu Zinabadilika?

Mafundisho ya Kiislamu ni mafundisho ya maana wala si ya dhahiri bila kuwa na maana yoyote. Kwa hivyo, mjadala wetu lazima uwe juu ya msingi wa maana na hekima. Ikiwa mafundisho ya Kiislamu yanatambulikana kwa sheria zake, hivyo, lazima tuangalie kwa kiasi gani sheria hizo zina sura ya kimaumbile. Vipi zinatabikiana na kukubaliana na muundo wa maumbile? Uislamu unafahamisha sheria. Sheria za Kiislamu zilizoelezwa, na Mwenyezi Mungu zimezingatia maumbile, binadamu na jamii. Sheria zimezingatia mfumo wa maisha ya binadamu. Kwa hivyo, tukitoa dalili hii yenye kuthibitisha kudumu kwa Uislamu (kama wanavyoandika waandishi wengi katika vitabu vyao kwa kutegemea msingi wa mabadiliko na msingi huo wa kifalsafa) hapana shaka tutaambiwa: "Ee Bwana! Maneno hayo si sawa. Kinachobadilika, kinachokuwa kikuukuu, kinachooza, kinachoharibika na kinachoangamia ni matukio (vitu)."

Sheria haingii katika hoja hii. Sheria lazima ijadiliwe kwa hoja tofauti. Kuna kikundi kingine kilicho afadhali kidogo. Kikundi hicho ingawa kinakubali kwamba sheria za maumbile hazibadiliki, lakini kinasema kwamba sheria zote zinazohusiana na maisha ya binadamu zinabadilika kwa kuwa maisha ya binadamu yanabadilika. Kwa dalili gani? Wanasema kwa sababu binadamu ni kiumbe ambaye ana jukumu juu ya nafsi yake mwenyewe, na kwamba kwa kuwa maisha na mahitaji ya binadamu yanabadilika, hivyo, sheria huwekwa ili kukidhi mahitaji yake. Hii ni shabaha ya sheria. Sheria huonyesha njia ya kutimiza haja za binadamu kiheshima na kiadilifu. Hivyo, msingi wa sheria ni kutosheleza mahitaji ya kijamii.

Sasa tuje kwenye suala la mahitaji. Je, mahitaji ya binadamu ni ya namna moja daima au yanabadilika? Mahitaji ya binadamu yanabadilika. Mahitaji ya binadamu katika zama za uvuvi yalikuwa ya namna moja na katika zama za uwindaji yalikuwa ya namna nyingine. Na katika zama zetu za mashine mahitaji ya binadamu ni ya namna nyingine kabisa. Kwa kawaida, ikiwa mahitaji ya kila zama yatabadilika, vivyo hivyo, sheria lazima zibadilike. Hii ina maana kwamba mahitaji ya kila zama yatatofautiana.

Tuchukulie mfano mmoja. Je, katika miaka mia moja iliyopita, binadamu alihitajia sheria za trafiki? Kwa mfano, sheria za barabarani za kuendesha upande wa mkono wa kulia au kushoto; kupiga faini kwa kosa la kitrafiki, n.k. Hapakuwepo haja ya kuwepo sheria za trafiki katika zama za punda kwa sababu hapakuwepo tatizo la trafiki katika mawasiliano ya watu. Suala la trafiki limezushwa na magari.

Sheria nyingi za kimataifa hazikuhitajiwa zamani, k.v. sheria za kimataifa za vyombo vya baharini. Haya ni mahitaji mapya na sheria mpya. Sheria zinazohusu mawasiliano ya angani ni sheria zinazohusu mataifa yote na zinakubaliwa na watu wote. "Kwa kuwa mahitaji yanabadilika hivyo sheria lazima zibadilike pia."

Hapana shaka kwamba maneno haya hayahusiani na hoja yetu. Hata hivyo, ni lazima tuzungumzie juu ya suala hili. Ingawa ni kweli kwamba wakati mazingira ya binadamu yanapobadilika mahitaji yake hubadilika pia, lakini suala lenyewe si rahisi kama linavyoelezwa kwa maneno hayo. Kwa nini? Kwa

sababu binadamu ana mahitaji yaliyo thabiti na ya siku zote, na mahitaji yanayobadilika na ya muda maalum tu. Si mahitaji yote ya binadamu yanayobadilika. **Mahitaji yanayohusiana na maana na shabaha ya maisha ya binadamu ni mahitaji yaliyo thabiti**, na mahitaji yanayohusiana na muundo (sura au mazingira) wa maisha ya binadamu ni mahitaji yanayobadilika na kugeuka.

Huwezi kuchukulia kubadilika daima kwa muundo wa maisha ya binadamu kuwa ni dalili ya kubadilika kwa maana na roho ya maisha ya binadamu. Mambo ya kidini yanahusiana na roho na msingi wa maisha wala hayahusiani na muundo wa maisha. Ukichungua mafundisho ya Kiislamu hutaona kwamba yanatilia mkazo muundo wa maisha. Huwezi kusema kwamba muundo wa maisha ubaki thabiti bila ya kubadilika. Uislamu unaupa uzito maana na roho ya maisha. Nimetoa mfano wa binadamu kuhusu suala hili. Ulimwengu pia uko katika hali kama hii.

Suala la Uthabiti na Ubadilikaji

Kusema kwamba kila kitu ulimwenguni kinabadilika si sawa. Maumbile ni sura ibadilikayo ya ulimwengu. Lau ulimwengu haungekuwa na sura iliyo thabiti basi kusingewezekana kuwepo sura ibadilikayo. Ikiwa kila kitu kitabadilika kama alivyoitakidi Heraclitus hapo zamani na itikadi yake ikafuatwa na watu wengi – basi hakutabaki kitu chochote kuwa sawa katika nyakati mbili wala hapatakuwepo uhusiano wowote kati ya zamani na sasa; hivyo, hapatawezekana kuwepo kanuni yoyote ulimwenguni. Ukweli ni kuwa ulimwengu huu una maumbile yanayobadilika na kwa wakati huohuo pia una hali iliyo thabiti ambayo ndiyo inayohifadhi hali ibadilikayo ya ulimwengu huu. Lau isingekuwepo hali igeukayo, hali thabiti isingekuwepo pia.

Wanafalsafa wa Kiislamu ambao walizungumzia suala la mwendo wa atomi (harakati za johari) wakati huohuo walizingatia pia sura thabiti ya ulimwengu. Walisema kwamba ingawa maumbile yanabadilika lakini yana roho ambayo daima ni thabiti.

Kwa ufupi, katika ulimwengu mzima kuna mambo yaliyo thabiti katika sura na hali ibadilikayo. Tuangalie viwiliwili vyetu vyenyewe – lau tusingekuwa na roho au maisha isiyotetereka au miliki maalum, basi viwiliwili navyo pia visingebadilika. Sisi ndisi; ndio wanadamu wenyewe tuliokuwepo miaka arobaini, hamsini, sitini au sabini iliyopita ingawa viwiliwili vyetu vilibadilika mara nyingi sana. Baadhi ya viwiliwili vyetu vilikauka na kutoka. Kwa mfano, sehemu moja ya viwiliwili vyetu iligeuka kuwa kucha; kucha tukazikata na kuzitupa katika madebe ya taka. Na sehemu nyingine ya viwiliwili vyetu ilikuwa katika umbo jingine kama seli za ngozi zetu, zikakauka na zinatoka. Mwenyezi Mungu anajua hivi viwiliwili vyetu miaka kumi iliyopita vilitupwa katika madebe ya taka gani, au katika vyoo gani; au mahali gani? Lakini tuishio ndio sisi, kwa kuwa roho zetu zimebaki.

Maisha ya kijamii ya binadamu yamefanana sawasawa na viungo vya binadamu. Vivyo hivyo kwa ulimwengu – vyote vina roho thabiti (isiyobadilika) na maumbo yabadilikayo.

Binadamu tangu zama za zamani amekuwa na haja ya kuyawekea maumbile yake nidhamu na utaratibu. Binadamu alikuwa na maumbile ya kuashiki, kupenda cheo na maumbile mengine mbalimbali.

(Ni suala jingine ikiwa vyanzo vyake ni vimoja au tofauti). Alikuwa nayo maumbile ya kijinsia, ya kutafuta elimu na kuchunguza; maumbile ya uzuri, wema, ihsani, maadili na maumbile ya kuabudu. Lakini binadamu alihitaji maumbile yote hayo yawe na nidhamu na utaratibu mmoja. Na nidhamu hiyo inaitwa maadili (*akhlaq*). Maadili ni tofauti na adabu. Kile kinachohusu utoaji wa mpango mzuri wa kutenda jambo, yaani nidhamu haibadiliki. kwa mfano, miongoni mwa misingi ya ulezi katika binadamu ni kuifanya akili ndiyo yenye kutawala matamania na matakwa ya binadamu. Wahenga wamesema kwamba “**Akili itawale nafsi.**” Hii ni kanuni moja kwamba kiwiliwili kinazeeka na maumbile ya ulimwengu yanakuwa makuukuu pia. Kanuni hii au msingi huu hauwi mkuukuu.

Kwa mfano, unaweza kusema kwamba: “Ni jambo zuri kwa binadamu kujitetea.” Haya ni maadili ambayo hayawezi kuwa makuukuu hata ikipita miaka elfu moja. huwezi kusema kwamba: “Zamani lilikuwa jambo zuri mtu kujitetea na kuvumilia lakini sasa si jambo zuri mtu kujiamini mwenyewe au kujitegemea mwenyewe.” Mambo haya hayawezi kubadilika. Mambo mengine yote ya kijamii, k.v. kusema kweli na kutosema uwongo, kuwa mwaminifu na kutofanya hiana, uadilifu, uhuru, usawa na kadha wa kadha, yote haya yanahusiana na roho au uhai wa maisha, hivyo hayawezi kubadilika.

Je, unaweza kusema kwamba ilivyokuwa dunia ya leo ni dunia ya kisasa, hivyo haiwezi kukubali maneno hayo? kwa hivyo, uadilifu, usawa na kupendana kumekuwa kuukuu? Tunaona leo kwamba kila taifa lina historia yake ambayo alikuwepo mtu miongoni mwao aliyesimama kupigania uadilifu, usawa na uhuru miaka elfu kadhaa iliyopita. Je, tunaweza kusema kwamba kupigania kwake kulikuwa bure? Hapana shaka hakukuwa bure kwani aliyoyapigania yalikuwa ni mambo yaliyohusu roho ya maisha wala hayakuwa umbo au sura ya maisha.

Binadamu na Mahitaji ya Zama

Suala hili tunalizungumzia hapa kwa kugusia tu. Kwa hivyo, ikiwa mtu atataka kutuambia kuhusu suala hili kwamba mahitaji ya binadamu yanabadilika, sisi tutamjibu kwamba: "Ndiyo, lakini si kama unavyosema wewe. Binadamu ana mahitaji ya aina mbili. Mahitaji yaliyo thabiti na ya daima, na mahitaji yanayobadilika. Kwa hivyo, si sawa kwa jumla kuwa mahitaji yanabadilika."

Uislamu unasemaje kuhusu mahitaji yaliyo thabiti na yanayobadilika? Nitalizungumzia suala hili katika sehemu nyingine ya mjadala wangu. Sasa tunataka kulizungumzia suala jingine, nalo linahusu mifano michache ya falsafa ya Ulaya na hasa falsafa ya [mwanafalsafa George Wilhelm Friedrich] Hegel [1770–1831] ambayo inaipa umuhimu mkubwa suala la utaifa na ukabila. Hegel ameliita suala hilo "Utovu wa Kukosea Zama" – yaani zama ina hali ambayo haikosei.

Hegel anaitakidi kwamba utaifa au roho ya taifa moja daima huenda mbele na huongozwa na akili kamilifu. Kwa hivyo, roho ya taifa haiwezi kukosea. Mtu anaweza kukosea lakini roho ya taifa haiwezi kukosea. Kwa maana nyingine, roho ya zama haiwezi kukosea. Baadhi ya wanafalsafa licha ya roho ya zama wanaitakidi kwamba hata roho ya jamii ya kibinadamu haikosei pia! Mambo haya vipi?

Ni lazima hapa niseme kidogo kuwajibu mabwana hao kwamba suala hasa si hilo wanalolizungumzia

wao, bali suala lenyewe ni hili, kwamba: Zama si kitu ambacho tunaweza kusema kwamba chenyewe kinakosea au hakikosei. Kinachotolewa na binadamu katika jamii kinatofautiana. Baadhi ya wakati maua huchanua kwenye akili, elimu, utafiti na uchunguzi wa binadamu. Hayo ni mambo ambayo ingawa huenda binadamu kwayo akakosea lakini kwa wastani tukiyatilia maanani tutaona kwamba kila binadamu anavyozidi kuendelea mbele basi makosa yake hupungua na huelekea kwenye kutafuta uhakika. Matukio ya kila zama ambayo ni matokeo kamili na halisi ya elimu, utafiti na akili ya binadamu ni lazima yatabikiane (yalingane) na ulimwengu. Ni muhali katika baadhi ya sehemu binadamu asijisawazishe na dunia, kwani hawezi kushindana nayo.

Chombo kipya kinapoundwa lazima kiwe rahisi, kiwe na nguvu zaidi na kudumu zaidi. Katika ulimwengu wa uchumi; yule mtu anayetumia gharama kubwa kutengeneza vitu kwa kutumia chombo cha kizamani kisha ikambidi aviuze kwa bei ghali, hawezi kabisa kushindana na yule mtu anayeua vitu kwa bei rahisi. Kwa hakika, haya ndiyo mambo yanayohusiana na ulazima wa kihistoria (historical determinism). Na hakuwezekani kukabiliana na kushindana na ulazima wa kihistoria.

Kwa mfano, ikiwa katika dunia hii ya kisasa iliyojaa zana na silaha za kivita itatokea nchi ambayo itaonyesha ukaidi wake kwa kutaka kutumia silaha za kivita za zamani, k.v. panga na mikuki, ili kuilinda nchi yake, hapana shaka yoyote kwamba kitendo hicho hakitachukuliwa kuwa ni ulinzi wa nchi, bali ni kusalimu amri. Haiwezekani kabisa silaha za kizamani ziweze kushindana na silaha za kisasa ambazo kila siku hubadilika.

Lakini pana jambo moja hapa ambalo ni lazima tuliielewe. Nalo ni kuwa binadamu si kiumbe cha pekee katika ulimwengu huu, wala si kweli kwamba vitendo vyake vyote vinatokana na maumbile yake ya kielimu. Binadamu ni kiumbe mwenye hawaa, matamania na tamaa pia. Vitu vingi sana vimetokeza katika dunia na vingi vyao ni vipya. Lakini ikiwa tutavichunguza kuona kama vitu hivyo vimetokana na akili na elimu ya binadamu au tamaa, uroho na hawaa yake, tutaona kwamba vitu hivyo havikutokana na elimu yake bali vilitokana na tamaa, uroho na hawaa ya binadamu, kwani hata kile kitu kilichotokana na elimu na sayansi kimo mikononi mwa watu wenye tamaa na hawaa.

Nakutoleeni mfano mmoja. Heroini (kasumba) ni tukio jipya au kitu kipya kabisa kilichotokeza na kuenea duniani. Heroini ni matokeo ya elimu, lakini si elimu huru. Heroini si matokeo ya elimu au akili bali ni matokeo ya elimu iliyotiwa mikononi mwa nafsi zenye hawaa na tamaa. Je, haya mabomu ya atomiki na silaha haribifu si matunda ya dunia ya kisasa? Basi kwa nini hata madola makubwa yenyewe yanafanya mikutano kushauriana jinsi ya kupata utatuzi wa kuzuia utengenezaji wa silaha hizo? Viongozi wa madola makubwa wanakaa pamoja ili kufikia mwafaka wa kuziangamiza silaha kali zinazoleta hasara na maafa makubwa. Hawasikilizani kuwa wengine watengeneze silaha kali na wengine wasitengeneze. Mikutano hiyo ya kuzuia silaha ina maana gani? Ina maana kwamba wao wenyewe wanahakikisha kuwa wameiendesha kombo na wameipotoa elimu (sayansi).

Vitu vingi vimevumbuliwa, k.v. atomi, umeme, jenereta, baruti, n.k. Wavumbuzi wa asili wa vitu hivi wamevivumbua vitu hivyo kwa lengo kwamba vitoe huduma na manufaa kwa wanadamu. Mmesoma

kwamba yule mvumbuzi wa baruti (Alfred Bernhard Nobel (1833–96)] alipoona kwamba baruti inatumiliwa vibaya alihuzunishwa sana kwa kadiri kwamba akaanzisha taasisi moja kwa ajili ya kutoa zawadi za Nobel kwa watu watakaotoa huduma zenye faida ili kufidia kitendo chake. Je, hamjasikia mara kwa mara habari za mwanasayansi mkubwa katika ulimwengu huu, Albert Einstein [1879–1955] ambaye amefariki katika zama zetu? Einstein alikuwa daima akisikitika kuona kwamba uvumbuzi wake katika mambo ya atomi ulitumiliwa vibaya hata kabla ya watu kunufaika nao. Alikuwa akisema: "Afadhali kama nisingekivumbua kuliko sasa kutumiwa na watu wenye tamaa na matamaniao."

Kwa hivyo, kuna uwezekano wa kuendelea au kupotea binadamu katika zama hizi. Sisi hatuwezi kukubali maneno haya kwamba ni lazima tujitabiki na kujirekebisha na mahitaji ya zama. Lazima hapa tufafanue kwamba mahitaji ya zama maana yake ni mahitaji na maisha ya binadamu. Je, mahitaji yepi tunayoyakusudia? Je, kila kitu kipya au kilichovumbuliwa katika karne hii ni kizuri? Au kila kitu cha zamani hakipendezi na hakifai tena? Haya si maneno sawa kusema kwamba katika dunia ya leo kitu hiki kinafaa na kupendwa au kitu kile hakifai au hakipendwi. Kupendwa au kutopendwa kitu kipimo chake si dunia hii. Dunia ya leo maana yake ni watu walio wengi. Watu walio wengi hawawezi kuwa mizani. Lazima tuvipambanue vitu vipya vya zama hizi. Sisi tu huru.

Aya ya Qur'ani inasema:

"Kwa hakika sisi tulivipa amana mbingu na ardhi na milima, lakini vikakataa kuichukua na vikaigopa; lakini mwanadamu akaichukua. Hakika ni dhalimu mkubwa, mjinga sana." (Qur'an 33:72)

Binadamu amechukua amana hiyo ambayo ni dhima na jukumu kubwa linalomtaka afuate mkondo wa zama na asipinge maendeleo ya zama. Asiwe mwenye kupendelea mambo ya kizamani kama walivyo baadhi ya watu. Lakini wakati huohuo ana jukumu jingine kubwa, nalo ni kupambana na upotofu wa zama.

Hapa panajitokeza jukumu la tatu, nalo ni kutambua na kupambanua baina ya maendeleo ya zama na upotovu wa zama. Tusiwe mfano wetu kama wale watu ambao wanapinga maendeleo ya zama eti ni upotovu, au wale wanaounga mkono upotovu wa zama eti ni maendeleo. Ikiwa sisi tunajihesabu kuwa ni walinzi wa mafundisho ya Kiislamu, basi ni wajibu wetu kupambanua njia ongofu katika jamii kwa kuielewa vizuri misingi ya kisayansi na kifalsafa ya jamii na kwa kusoma sana historia. Kwa kufanya hivyo ndipo tutakapoweza kupambanua baina ya kikundi kiaminifu na kikundi kiharibifu. Tutaweza kupambana na kile kikundi kinachopinga kila kitu kipya au jambo jipya.

Wako baadhi ya watu ambao wameng'ang'ania kwa kusifu kila kitu cha kizamani. Kwa mfano, wako baadhi ya watu wanapendelea kutumia kalamu ya zamani yenye umbo maalum pamoja na dawati lake, kila wanapoandika wawe wakichovya wino. Huko ni kuchukua taabu na kupoteza wakati. Inatosha mtu atumie kalamu ya wino ya kawaida ambayo atajaza wino mara moja kisha ataandikia kwa saa kadhaa. Hatokuwa na haja tena ya kufikiria wino uko wapi na kila mara awe akichovyachovya. Kidau (kidawati) kilikuwa cha zama za mababu zetu. Kwa hivyo, haielekei tuache kutumia hii kalamu ya kisasa na

tushikilie kalamu ya kizamani. Jamaa mmoja aliyekuwa akiwakejeli watu wenye kutumia vitu vya kisasa na kuviacha vya kizamani, alikuwa akisema: "Wanaacha kupanda punda wa Mungu wanapanda motokaa ya shetani!"

Wakati taa za umeme zilipoanza kutumiwa, watu wengi ambao hawakuona kwa mara ya kwanza walipinga. Mimi mwenyewe sikumbuki, lakini nimehadithiwa kwamba wakati taa za umeme zilipowashwa mjini Mash'had, mtu mmoja alianza kufanya ghasia kupinga na watu wakaja na wakazizima. Kwa nini? Kwa sababu gani? Kwani miongoni mwa aya za Qur'ani kuna aya inayosema: "Enyi mlioamini! Nakuusieni kibatari. Msije mkaacha kutumia kibatari cha mafuta ya taa mkafikwa na balaa!!"? Ama kuna aya nyingine inayosema: "Enyi mlioamini! Nakuusieni daima pandeni punda wala msipande kitu kingine!!??"

Hii ni desturi iliyozoewa na watu kisha ikapewa sura ya kidini. Kuna kisa kingine ninachokikumbuka cha bwana mmoja wakati shule zilipokuwa zikifunguliwa mikoani. Bwana huyo alikuwa akifikiri kwamba kama hutosoma chuoni (madrasani) hutoweza kuwa shekhe (mulla). Alikuwa akisema: "Mambo gani haya? Kwani watoto wasomapo chuoni hawawi mashekhe? Kwani Sheikh Murtadha Ansari kwa kusoma alif, be, chuoni hajawa shekhe mkubwa? Kwa hivyo, watoto wetu wakisoma vyuoni na madrasani watakuwa wanavyuoni lakini hawatokuwa hivyo wakisoma shuleni." Bwana huyo alikuwa akifikiri kwamba Sheikh Murtadha Ansari amekuwa mwanachuoni mkubwa kwa sababu ya kusoma chuoni peke yake. Ingawa chuo hakikuwa kizuizi kikubwa kwake lakini lau masomo yake angefundishwa kwa mpango bora zaidi basi hapana shaka angekuwa mwanachuoni mkubwa zaidi.

Haya si miongoni mwa mafundisho ya Kiislamu kwamba tukitaka kuwafunza watoto wetu ni lazima tuwafunze kwa utaratibu wa alif, be, n.k. Uislamu haukutilia mkazo mbinu hizi.

Source URL:

<https://www.al-islam.org/sheria-za-kiislamu-katika-dunia-ya-kisasa-murtadha-mutahhari/mabadiliko-katika-kilichotukia>